N13/2/ABSWA/HP1/SWA/TZ0/XX/T

88132316

International Baccalaureate®
Baccalauréat International
Bachillerato Internacional

**SWAHILI B – HIGHER LEVEL – PAPER 1**
**SOUAHÉLI B – NIVEAU SUPÉRIEUR – ÉPREUVE 1**
**SUAHILI B – NIVEL SUPERIOR – PRUEBA 1**

Tuesday 12 November 2013 (afternoon)
Mardi 12 novembre 2013 (après-midi)
Martes 12 de noviembre de 2013 (tarde)

1 h 30 m

TEXT BOOKLET – INSTRUCTIONS TO CANDIDATES

- Do not open this booklet until instructed to do so.
- This booklet contains all of the texts required for paper 1.
- Answer the questions in the question and answer booklet provided.

LIVRET DE TEXTES – INSTRUCTIONS DESTINÉES AUX CANDIDATS

- N'ouvrez pas ce livret avant d'y être autorisé(e).
- Ce livret contient tous les textes nécessaires à l'épreuve 1.
- Répondez à toutes les questions dans le livret de questions et réponses fourni.

CUADERNO DE TEXTOS – INSTRUCCIONES PARA LOS ALUMNOS

- No abra este cuaderno hasta que se lo autoricen.
- Este cuaderno contiene todos los textos para la prueba 1.
- Conteste todas las preguntas en el cuaderno de preguntas y respuestas.

8813-2316

9 pages/páginas

© International Baccalaureate Organization 2013

Blank page
Page vierge
Página en blanco

**KIFUNGU A**

# MWANAFUNZI BORA NCHINI

Matokeo ya mtihani wa darasa la nane* yalipotangazwa hapo Desemba 27 mwaka uliopita, jambo la kwanza lilikuwa kutangaza mwanafunzi bora zaidi nchini. Nashangaa ni kwa nini Wizara ya Elimu iligeuza mtindo wa mbeleni ambapo wilaya iliyofanya vizuri ndiyo iliyokuwa ikitangazwa badala ya mwanafunzi bora.

Kwa maoni yangu, haina haja ya kutaja mwanafunzi bora. Hii ni sawa na kufedhehesha wanafunzi wengine waliofanya mtihani huo. Tena, mtindo huu hauwezi kuwatia motisha watahiniwa kutia bidii masomoni kwa vile si rahisi kwa wanfunzi wote kufikia kiwango kama hiki.

Mtindo huu wa kutaja wanafunzi bora nchini bila shaka una dosari kubwa. Kwa mfano, ikiwa sijakosea, wengi wa wanafunzi ambao wamewahi kutajwa kama mashujaa wametoka kwa shule za kibinafsi. Na tujuavyo, ni kwamba shule hizi zinamilikiwa na matajiri na wanafunzi pia wazazi wao ni matajiri. Hivyo basi kwa kuwataja wanafunzi hawa ni dhahiri kuwa utajiri ndio unaodhihirisha kwamba unaweza kutoa elimu bora.

Hii ni njia mojawapo ya kudunisha elimu ya shule za umma na tena kudunisha elimu ya baadhi ya wanafunzi wanaotoka katika jamii maskini. Si hayo tu, hii pia ni njia mojawapo ya kutuza familia ya mwanafunzi huyo. Na wazazi wa wanafunzi kama hawa, huonekana kana kwamba ndio wanaoweza kusomesha vizuri zaidi.

Isitoshe, nasikitika kusema kwamba wakati huu ambapo serikali imetupa elimu ya bure, kuna baadhi ya wanasiasa na matajiri wengine ambao hawafurahii elimu hii ya bure. Na ndipo utaona kwamba wakiona wanafunzi bora na shule bora ni za watu binafsi, watachukua nafasi hii kupiga vita elimu ya bure na vilevile shule za umma. Hapa ndipo vita vya maskini na tajiri vitatokea.

Ombi langu ni kwa Waziri wa Elimu na ambaye pia alitangaza matokeo hayo, ageuze mtindo huu na badala yake awe akitangaza wilaya bora tu, ili tangazo kama hilo lishangiliwe na wilaya nzima lakini kutaja mwanafunzi bora tu, hii ni sawa na kutuza familia moja tu. Na ndipo hapo majivuno na kinyongo hujionyesha wazi kutoka kwa familia husika.

Wizara ya Elimu haina budi kubadilisha mtindo huu wa kupotosha na kutekeleza wajibu wake kwa Wakenya.

*Taifa Leo* (2004)

* nane: mtihani wa darasa la nane nchini Kenya

**KIFUNGU B**

# SIMU TAMBA

Uvumbuzi wa simu tamba au rununu ni uvumbuzi ambao tunaweza kusema kuwa ni mkubwa sana katika karne hii baada ya uvumbuzi mwingine kama wa magari na runinga. Vifaa hivi vyote hutumika kwa kueneza ujumbe kutoka mahali pamoja hadi pengine.

Simu tamba ni suluhisho kwa matatizo mengi ambayo waja walikuwa wakikumbana nayo. Simu tamba zinatuwezesha kuwasilisha mambo ya umuhimu kwa njia ya haraka. Hebu fikiria kuna mtu ambaye maisha yake yamo hatarini lakini inakubidi upige foleni ili uweze kupiga simu! Siku hizi mambo kama hayo yamewekwa katika buku la sahau. Kutokana na uvumbuzi wa rununu kwani ujumbe wa haraka huweza kuwasilishwa moja kwa moja. Kabla ya uvumbuzi wa rununu au simu tamba maisha ya watu yangepotea kutokana na ukosefu wa mawasiliano bora. Kwa hivyo simu tamba ni suluhisho!

Simu tamba ni suluhisho kwa wale wanaoishi mashambani ambako simu za wakati huo kawaida hazikuwepo. Uvumbuzi huo umempa kila mtu fursa ya kuwasiliana na yeyote, si nchini tu bali hata katika nchi zingine.

Huwezi kukosa kupokea ujumbe wowote eti kwa sababu ulikuwa mahali fulani. Hivi vidubwasha huwekwa hata vikapuni unapoenda shambani! Siku hizi uandishi wa barua ni nadra sana kwa sababu ujumbe unaweza kuwasilishwa kwa kutumia simu tamba.

Rununu pia ni vifaa vya kujiburudisha navyo. Aina nyingi za rununu zina michezo ya aina nyingi ambayo unaweza kuicheza wakati wowote ule. Isitoshe unaweza kupata ujumbe kupitia kwa njia ya mtandao.

Kuna aina nyingine ya rununu ambazo zina kamera. Mtu anaweza kupiga picha na kuhifadhi ili aweze kuzitazama wakati wowote. Panapokuwa na haja kuna picha za muhimu ambazo zinafaa kurejelewa kila mara, siyo lazima tena uziweke kwenye vitabu vya picha. Rununu inatupa fursa ya kutuma ujumbe kwa ada ndogo sana. Ujumbe hufika wakati uo huo.

Rununu pia zina tarakilishi ndogo ambayo hurahihisha mawasiliano, kwa njia ya mtandao. Licha ya hayo, simu hizi zina shajara na kifaa cha kukumbusha iwapo unahitajika kuwa mahali popote na kile ambacho unahitajika kufanya. Heko kwa uvumbuzi huu kwa sababu swala la kusahau kuhudhuria mikutano halipo tena.



Simu tamba inafanya mtu kuweza kuwasiliana na yeyote mahali popote wakati wowote kwani ni ndogo, na mtu huenda nayo popote aendapo, na ndiyo sababu inaitwa simu tamba.

Hata hivyo simu hizi huchukiza wakati mwingine. Hebu tuchukulie mfano wa mwenyekiti ambaye alikuwa akiongoza mkutano kisha akapokea simu. Labda mwenyekiti alikuwa akiiongojea simu na akafikiria kwamba ingepigwa kabla ya mkutano kuanza. Huenda ikawa simu yenyewe ni ya dharura kwa hivyo hatakuwa na lingine ila kuipokea. Je, na hao wengine ambao walikuwa kwenye mkutano watafanya nini? Wataachwa tu katika hali ya taharuki.

Isitoshe, huenda ikawa unashughulikia jambo ambalo ni muhimu sana ofisini mwako ambapo hata sauti ya mbu pekee ingeudhi. Kisha unapokea simu ambapo mwandani wako anataka tu mpige gumzo au akuarifu jinsi mtakavyoenda kutazama filamu fulani.

Ni usiku wa manane, umelala usingizi wa pono. Mara mlio wa simu. Mtu amekupigia simu kisa na maana ni kuwa ni wakati malipo ya simu ni ya chini. Lakini je, mbona umharibie mtu usingizi wake eti kwa sababu malipo ya simu ni yamepungua? Unapokuwa kanisani kasisi anahubiri au mko katikati ya maombi. Mara unasikia mlio wa simu. Hali hii huleta utata kwa hadhira yote.

Ingawa kuna hila zinazoletwa na utumizi wa simu tamba, simu tamba zimetufanya tupige hatua katika sekta mbalimbali. Tuzielewe na tuzitumie kwa makini.

K Collins *et al.*, *Johari ya Kiswahili* (2004)

**KIFUNGU C**

# UWEJE UONEKANE UMEPENDEZA?



Kuchagua mavazi, kulinganisha vazi gani linakufaa kwa ajili ya wakati na mahali unapokwenda au hata kuvaa tu katika hali ya kawaida, ni jambo linalowasumbua watu wengi hasa wanawake ingawa ni tatizo pia linaathiri wanaume "wanaojipenda".

Linatokea pale mtu anapotaka "kujipanga" kutaka kutoka, pengine kwenda harusini au kwenye sherehe inayokusanya watu wengi. Katika hali kama hiyo, mvaaji mara nyingi atapangilia mavazi atakayovaa kwa sherehe hiyo.

Inapotokea hali kama hii akili ya mvaaji huwa katika hali ya kuchanganyikiwa na kwa sababu hiyo huenda asivae mavazi yanayompendeza tena na akavaa bora kuvaa. Hali hii hutokea hasa kwa mtu aliye pekee.

Jambo hili pia hutokea katika hali nyingine, kwamba mtu anapokuwa anatafuta mpangilio mzuri wa mavazi pengine anakuwa na mtu mwingine pembeni yake au watu wengine ambao ni watu wake wa karibu na anawaamini kiushauri.

Katika ile hali ya kuchagua na kuamua avae nini kwa "mtoto wake" inatokea wenzake wanamshauri au kumwambia kuwa mavazi aliyovaa hayakumpendeza au hayaendani kwa sababu hiyo wanamshauri avae mavazi mengine badala ya hayo. Hao wanaomshauri wanamshauri kwa sababu ya kuona mpangilio wa mavazi yake na muonekano wake kwa wakati huo na kwa macho yao wanahisi kabisa si mpangilio mzuri unaompendeza na kwa sababu hiyo ndipo wanapotaka ushauri huo kwa faida yake.

Katika hali kama hii ndipo swali linapozuka hivi mtu ili aonekane amependeza ni nini kinahitajika? Ni kuridhika yeye binafsi kwa muonekano alio nao kimavazi na kimapambo? Ni muonekano ambao unavutia watu wengine wanaomwangalia au ni nini?

George Mponda, fundi mshoni mkazi wa Kariokoo anasema, mara nyingi hali ya watu kupata taabu katika mpangilio wa mavazi na kuhisi kama wamependeza au hawajapendeza kutokana na uchaguaji wa rangi za nguo. Anasema: "Kuna aina ya nguo zenye rangi ambazo ukitaka kuzitumia unapaswa uwe mjuzi wa mpangilio wa mavazi. Nguo zenye rangi zaidi ya tatu, hizi zinahitaji umakini sana hasa na mara nyingi zinatumiwa na wanawake, mvaaji anatakiwa awe stadi wa kupangilia."

"Utata wa nguo za kitambaa cha rangi nyingi ni kwamba zinachagua sana rangi ya ngozi ya mtu, sasa utakuta mtu ameona mwenzake amevaa nguo ya aina hiyo na yeye akaipenda, akaenda, kununua bila ya kujua kuwa rangi yake na nguo hiyo haviendani. Huyu hatapendeza."

Tofauti kidogo na Mponda, Denis Munga mtaalamu wa masuala ya saikolojia yeye anasema kinachotokea katika hili ni suala la hisia zinazoongoza akili katika mvuto wa mavazi ambao unapotokea na kuiathiri akili ndipo humuongoza mtu kuhisi kupendeza kwake ni kuvaa vazi gani.

"Chukulia hawa vijana wanaovaa milegezo," anasema Munga na kuendelea, "hawa katika hisia zao wanaona kuwa wamependeza ingawa machoni mwa watu wengi mavazi yao ni kioja."

*Nipashe* (2012)

**KIFUNGU D**

# MAISHA YA MJINI

Mtaa wa Watoro, walikoishi Neema ni baadhi ya mitaa iliyojengwa kwa ajili ya watu wa mapato ya chini jijini humo, kuambatana na mwito wa serikali iliyochukua mamlaka baada ya kipindi cha ukoloni wa "nyumba bora kwa kila mwananchi". Mtaa wenyewe ni milki ya manispaa ya jiji. Licha ya kwamba ulijengwa kwa ajili ya watu wa mapato ya chini, wakati huu ni sawa na mtaa wa watu wenye mapato ya kadri. Ulianza kuvamiwa na watu wenye uwezo baada ya miaka kadhaa ya maisha kupanda kwa kiwango hadi kuwashinda wengi kuyamudu. Isitoshe, watu wengi walizidi kugura mashambani, wakija kurundikana jijini, jambo lililosababisha upungufu mkubwa wa makao. Ni wakati huo ambao wale hohehahe wa jijini waliokuwa wakaazi halali wa mitaa kama ile ya Watoro, walipotekwa na mawimbi ya uchumi mgumu, wakasombwa mmoja baada ya mwingine, wakienda kusalimikia katika mitaa ya mabanda, iliyoanza kuchipuka usiku na mchana. Kwa sasa mtaa wa Watoro sio tena makaazi ya watu wenye uwezo wa kadri, wengi miongoni mwao wakimiliki hadi na fahari za magari.

Harry ni kijana aliyeinuka. Umri wake ni miaka ishirini na saba. Baada ya kumtunga mimba Neema, wakati msichana akiwa angali mwanafunzi katika kidato cha pili, alilazimishwa kumtwaa, awe mkewe. Alipoingizwa katika ndoa bila kutarajia, alimcuhukua mpenzi wake mja mzito kwa moyo safi, kwa vile alimpenda vilivyo msichana mwenyewe. Bila kazi, alimkabidhi mkewe mikononi mwa mama yake kule mashambani, naye akarudi jijini kukisaka kibarua. Alisaidiwa na ndugu zake hadi kufaulu kuajiriwa katika kiwanda maarufu cha kugema matindi. Baada ya kupata kibarua, alirejea mashambani kwao, kwenda mchukua mkewe hadi jijini.

Harry mwenyewe ni mtu mwenye juhudi kazini. Ni mvumilivu na mnyenyekevu kwa wakubwa na wadogo zake. Hajui kujivisha ukubwa au mamlaka kazini. Husubiri kwa maombi na imani, madaraka yenyewe yamtafute. Tangu alipoajiriwa, amewaridhisha mabwana zake hadi kumpandisha ngazi mara mbili. Ndiyo sababu ya kuweza kuishi katika mtaa kama huo wa watu pato la kadri bila wahka ya kumkimu mkewe, mwenye shughuli za umama na mekoni pekee, na mwanawe wa umri wa miaka minne u nusu sasa. Ni mpole kwa mwenendo, asiye mjuzi wa kuzungumza jinsi alivyo Neema mkewe.

Ukimtazama Neema, licha ya kwamba hajui kutoka kwenda kutafuta bali kukaa akisubiri maisha mema kuletwa kwa uwezo wa mshahara wa mumewe, utamwona mama kijana aliyetulia kwa hali zote; hana dukuduku lolote. Kutokana na maisha kama hayo ya Harry na Neema, Korneli na Janeti (wageni wa Neema na Harry) walijawa na imani kuwa hata nao pia, yao yatanyooka baada ya kipindi kifupi cha kuishi jijini.

Alasiri yote hiyo kwenye gumzo, Neema aliwapa matumaini ya ufanisi mtupu wageni wake. "Msiwe na wasiswasi Janeti. Mtayazoea maisha, na mwishowe yatakuwa mazuri. Nitazame nilivyo sasa. Miaka mitano ya kisogoni, sikuota eti ipo siku hata nami nitaishi katika nyumba yangu mwenyewe, huru huria, kutenda nitakalo kwa wakati niutakao. Ufanisi kwa maisha yangu ulikuwa mbali kuzidi upeo wa macho yangu. Mume wangu alipotoka kurudi huku kuisaka kazi, nami nikiachwa mikononi mwa mama yake mzee, niliomboleza usiku kucha na mchana kutwa. Nikajuta kwa nini kuishika mimba hadi kulazimika kuacha shule. Sikuwa na kokote kwa kutorokea, kwa vile kwetu nyumbani, baba hakutaka kuniona popote karibu na hapo. Mkivumilia nanyi pia na kuweka bidii, mafanikio yenu hayako mbali sana."

Moses A Andere, *Uhondo Mchungu* (2005)

**KIFUNGU E**

# Umaskini Barani Afrika



"Mwenyekiti wa kamati Andalizi ya kongamano hili, mabibi na mabwana. Umaskini ndilo tatizo kubwa zaidi barani Afrika. Umaskini ni ile hali ya mtu kukosa chakula, makazi na uwezo wa kumiliki mali au kushiriki shughuli za kuzalisha mali. Nchini Kenya, mtu husemekana kuwa mkata iwapo pato lake ni chini ya shilingi 1,239 kwa mwezi. Umaskini umetopea barani Afrika kiasi kwamba 60% ya wakazi wake wametota katika dimbwi la uchochole. Dhiki kubwa ya hali hii inapatikana majijini ambamo watu wengi wanaishi katika mitaa ya mabanda.

Kuna mambo mengi yanayochangia kuwepo kwa umaskini. Moja ya mambo haya ni kuongezeka kwa idadi ya watu. Hivi sasa, kuna Waafrika milioni 800, wakiwemo Wakenya milioni 29. Jambo la pili, ni kuwa chumi zimeporomoka na mapato ya kitaifa ya nchi nyingi yamedidimia. Kwa hivyo, serikali zinashindwa kutoa huduma za kimsingi kama chakula, maji na afya kwa raia. Ili kujiokoa, nchi nyingi zimeamua kukopa kutoka nchi zilizoendelea. Baadaye, nchi za Kiafrika hulazimika kutumia fedha nyingi kidogo zinazopata kulipia riba huku wanachi waikiteseka.

Bwana mwenyekiti, jambo la tatu lichangialo ufakiri ni masharti yanayoambatana na mikopo. Nchi nyingi zimelazimishwa kuweka soko huru, kubinafsisha mashirika ya umma na kupunguza idadi ya wafanyikazi. Matokeo ni kuwa bidhaa kutoka nje zimeangamiza viwanda. Tena nafasi za ajira sasa ni finyu hata vijana wenye shahada za vyuo vikuu leo wanasaga lami mitaani wakitafuta kazi.

Umaskini Afrika pia unatokana na bei duni ya masoko ya nje. Bara la Afrika limekuwa likiuza rasilimali na mazao kwa nchi zilizoendelea kwa bei ya kijungu jiko. Hivyo, nchi za Afrika hazipati faida za kuweza kuimarisha hali ya maisha ya watu wake. Isisahaulike kuwa sisi wenyewe tunachangia umaskini. Hii ni kutokana na uongozi mbaya. Mipango ya maendeleo ya watawala wengi ni mibaya. Mfano wa hii ni ubadhirifu wa pesa kwa miradi ya kifahari kama viwanda vya silaha ambavyo havina faida."

Francis Watitui *et al.*, *Kiswahili Fasaha* (2005)